# WAMISIONARI WA DAMU AZIZI

## PROVINSI YA TANZANIA

# MWONGOZO WA UTUME WA WALEI WA DAMU AZIZI

# (UWADA)

**June, 2017 - Kisasa – Dodoma**

## YALIYOMO

**UTANGULIZI ........ 3**
**1. SEHEMU YA KWANZA ........ 4**
1.1. TAARIFA YA CHAMA ........ 4
1.2. UFAFANUZI WA MANENO ........ 4
**2. SEHEMU YA PILI ........ 4**
2.1. KARAMA NA NGUZO TATU ZA CHAMA ........ 4
2.2. MADHUMUNI ........ 4
**3. SEHEMU YA TATU ........ 5**
3.1. UANACHAMA ........ 5
3.1.1. Sifa za kuwa Mwanachama ........ 5
3.1.2. Masharti ya Uanachama ........ 5
3.1.3. Wajibu wa Mwanachama ........ 5
3.1.4. Haki za Mwanachama ........ 5
3.1.5. Ukomo wa Uanachama ........ 6
3.2. MALEZI ........ 6
3.2.1. Malezi ya Awali ........ 6
3.2.2. Kupokelewa Rasmi na Daima ........ 6
3.2.3. Malezi Endelevu ........ 7
**4. SEHEMU YA NNE ........ 7**
4.1. MUUNDO WA CHAMA ........ 7
4.2. UONGOZI ........ 7
4.2.1. Mfumo wa Uongozi ........ 7
4.2.2. Wajibu na Kazi za Viongozi ........ 8
4.2.3. Kusitishwa kwa Uongozi ........ 9
4.3. VIKAO ........ 9
**5. SEHEMU YA TANO ........ 9**
5.1. IBADA NA SALA ........ 9
5.2. UTUME ........ 10
**6. SEHEMU YA SITA ........ 10**
6.1. MICHANGO ........ 10
6.1.1. Mchango wa Kiingilio ........ 10
6.1.2. Ada ya Mwaka ........ 10
6.1.3. Michango Mingine ........ 10
**7. VIAMBATISHO ........ 11**
7.1. IBADA YA KUPOKELEWA WANACHAMA WAPYA ........ 11

## UTANGULIZI

### Utume wa Walei Katika Kanisa

a) Kimsingi, kila Mkristo mlei, na kwa hakika waumini wote kwa jumla, wamepewa heshima na Mwenyezi Mungu ya kushiriki katika adhama na kazi tukufu ya utume. Kila Mkristo ametunukiwa dhima hiyo kupitia sakramenti za Ubatizo na Kipaimara. kwa hiyo basi, kila mlei, ama kwa nafsi yake mwenyewe, au kwa kushirikiana na wenzake kupitia jumuiya kadhaa, ana haki na wajibu wa kutangaza ujumbe mtukufu wa ukombozi ili uweze kukubalika na kila mtu duniani kote (Mtaguso wa II wa Vatikani).

b) Wajibu huu unakuwa mkubwa zaidi pindi inapodhihirika kuwa mlei ndio njia bora zaidi ya kutangaza Injili na kulifanya jina la Kristo lijulikane kwa wote. Kwa kiwango kikubwa, shughuli zao katika jumuiya ya Kanisa ni muhimu sana kiasi kwamba bila mchango wao kazi ya viongozi wa dini peke yao haiwezi kufikia kiwango cha ubora kinachotakikana (Mtaguso wa II wa Vatikani).

c) Sakramenti ya ubatizo inamunganisha mlei na mwili wa Kristo, na hivyo kumuingiza katika jamii ya Watu wa Mungu. Kwa namna ya pekee walei wanakuwa washiriki katika majukumu ya Kristo ambayo yanajumuisha ukuhani, unabii na ufalme. Aidha wanatekeleza sehemu yao ya wajibu huu wa Kikristo katika Kanisa na katika ulimwengu pia (KKK 900).

d) Walei, kwa mujibu wa hadhi yao, huutafuta ufalme wa Mungu kwa kujishughulisha na mambo ya dunia na kwa kukabiliana nayo kulingana na mpango wa Mungu. Wanaishi duniani, yaani, kwa kulingana na taaluma na shughuli zao zilizo nje ya imani yao. Wanaishi katika mazingira ya kawaida ya kifamilia na kijamii-ambayo ndiyo kiini hasa cha uhai wao. Na ni ndani ya mazingira hayo hayo ambamo Mungu huwagusa ili watekeleze wajibu wao na kwa mwongozo wa nuru ya Injili waweze kuwa chachu ya kuutakasa ulimwengu. *(Lumen Gentium 31)*

### Utume wa Walei wa Damu Azizi

a) Shirika la Wamisionari wa Damu Azizi linatambua na kuhimiza Utume wa Walei wale wanaoshiriki nasi katika Tasaufi ya Damu Azizi kama baraka kwa Shirika na linathamini uwepo wao. Walei hawa wanaongozwa na katiba na miongozo yao kadiri ya mazingira (S 12).

b) Makundi haya ya walei yameibuka katika mazingira tofauti tofauti kutegemeana na mahusiano yaliyojengeka kati yao na Wamisionari wa Damu Azizi katika utume wao katika nyanja za miito au malezi, uchungaji wa kiparokia na katika taasisi mbali mbali za huduma za kijamii. Walei hawa wameguswa na Tasaufi ya Damu Azizi na wanahiari kushiriki katika utume wa damu kama njia mojawapo ya kujitakatifuza.

c) Kwa kutambua umuhimu huu wa walei katika utume wa Kanisa na Shirika, Wamisionari wa Damu Azizi, Provinsi ya Tanzania, kwa kushirikiana na walei wana utume wa damu, wameandaa mwongozo huu uwasaidie walei hawa kuuishi utume wao kikamilifu kwa kufuata karama ya Mt. Gaspari Del Bufalo.

## 1. SEHEMU YA KWANZA

### 1.1. TAARIFA YA CHAMA

a) Jina la chama litakuwa: **Utume wa Walei wa Damu Azizi**

b) Anuani ya chama: S.L.P. 932 DODOMA.

c) Eneo la shughuli za chama litakuwa mahali popote Tanzania na nje ya Tanzania kutegemeana na uwepo wa wanachama na mahitaji ya utume.

d) Makao Makuu ya chama yatakuwa: Dodoma.

e) Alama za Chama zitakuwa Tasbihi ya Damu Azizi, Kitabu cha Damu ya Kristo Mto wa Rehema na beji.

### 1.2. UFAFANUZI WA MANENO

a) "Chama" lina maana ya Umoja wa utume wa Walei wa Damu Azizi

b) "Mwanachama" ni mkristo yeyote mkatoliki aliyejiunga na chama na anayeshiriki kikamilifu kuuishi utume wa Damu Azizi kadiri ya mwongozo wa chama.

c) "Mwana utume wa Damu" ni jina litakalotumika kumtambulisha mwanachama katika maisha ya kila siku hata kama halijatumika sana katika mwongozo huu.

d) "Viongozi" ni wanachama waliochaguliwa au kuteuliwa kwa mujibu wa mwongozo huu, kusimamia uendeshaji wa utume wa chama.

e) "Mwongozo" ni machapisho haya yenye kanuni na mwongozo wa maisha ya wanachama katika kutekeleza madhumuni na malengo ya chama.

f) "Shirika" ni Shirika la Wamisionari wa Damu Azizi.

## 2. SEHEMU YA PILI

### 2.1. KARAMA NA NGUZO TATU ZA CHAMA

a) Karama ya chama itakuwa ni kuhubiri Neno la Mungu, kwa kusukumwa na Tasaufi ya Damu Azizi, kwa njia ya mafungo, semina, sala na utume wa kusikiliza na kuitikia kilio cha damu.

b) Nguzo za chama zitakuwa tatu: Maisha ya jumuiya yaani maisha ya uanachama ndani ya chama, Tasaufi ya Damu na Utume.

### 2.2. MADHUMUNI

a) Kushiriki katika fumbo zima la ukombozi kwa kufanya wengi wamfuate Kristo.

b) Kujitakatifuza wenyewe na watu wengine kwa njia ya sala, sakramenti na matendo ya utakatifu.

c) Kushiriki katika sala na ibada mbalimbali kadiri ya mwongozo wa chama

d) Kushirikiana na wachungaji wa parokia na majimbo mahalia katika shughuli mbalimbali za uchungaji kadiri ya maelekezo ya Kanisa kwa vyama vya kitume.

e) Kushirikiana na vyama na vikundi mbalimbali vya kitume na visivyo vya kitume katika shughuli zote za kusia, kukuza na kukoleza imani.

f) Kukemea matendo yote yanayohusisha ukandamizaji wa haki za binadamu, unyanyasaji, uonevu na matendo yote yanayodhalilisha utu wa mwanadamu hasa pale pasipo na mtu anayekemea.

## 3. SEHEMU YA TATU

### 3.1. UANACHAMA

#### 3.1.1. Sifa za kuwa Mwanachama

a) Awe ni mkristo mkatoliki mwenye umri kuanzia miaka 18 aliyepokea sakramenti tatu zinazomwingiza mtu kwenye ukristo (Ubatizo, Komunio na Kipaimara)

b) Awe ametimiza masharti na taratibu zote za kujiunga na chama kadiri ya mwongozo huu.

c) Awe ni mtu aliye tayari kuheshimu na kuufuata mwongozo wa chama

#### 3.1.2. Masharti ya Uanachama

a) Kutii mwongozo wa chama

b) Kuhudhuria vikao vyote vya chama

c) Kuheshimu na kutekeleza maamuzi ya chama

d) Kulipa ada na michango itakakayoamuriwa na chama

#### 3.1.3. Wajibu wa Mwanachama

a) Wajibu wa mwanachama umejumuishwa katika Yohana 15:13 itakuwa upendo zaidi ya ule wa mtu kutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake; mwanachama anaalikwa kufuata mfano wa Kristu wa kuutoa uhai wake kwa ajili ya watu wengine.

b) Kufanya jitihada za kujitajirisha katika uelewa wa Neno la Mungu na mafundisho mengine ya Kanisa kwa njia mbalimbali kama: Kujisomea, semina, mafungo, sala, ibada n.k.

c) Kuunganika zaidi na Kristo kwa kushiriki mara kwa mara fumbo la Ekaristi Takatifu kwa kufuata utaratibu wa chama mahali kilipo.

d) Kujitakatifuza kwa kushiriki sakramenti ya kitubio na upatanisho mara kwa mara pia kuwasaidia wengine waoshwe dhambi zao kwa Damu Azizi ya Kristo.

e) Kusali kibinafsi na katika chama sala mbalimbali kama zilivyoelekezwa na Kanisa au chama kwa wokovu wa wanachama na taifa zima la Mungu.

f) Kujiunga na kuendelea kuishi katika jamii ya waumini katika Kanisa kuanzia kwenye jumuiya ndogondogo ili kuujenga Ufalme wa Mungu hapa duniani.

g) Kushiriki katika shughuli zote zinazosaidia kuleta amani, haki na upendo hasa kuwasemea na kuwatetea wanyonge wanaokandamizwa na wengine, ili waonje upendo wa Mungu maishani mwao.

h) Kuwa tayari kuwashirikisha wengine hata kile kidogo alichonacho mwanachama ili kwa njia hiyo kujiwekea hazina isiyoharibika mbinguni.

i) Kuishi kwa kufuata mfano wa Yesu, Bikira Maria, Mt. Gaspari na ya watakatifu wengine waliopita duniani.

#### 3.1.4. Haki za Mwanachama

Mwanachama atakuwa na haki zifuatazo:

a) Kutumia na kupata huduma zote za chama bila ubaguzi

b) Kupokea taarifa za chama, kuona taarifa au kumbukumbu za chama kwa utaratibu unaokubalika.

c) Kuchagua (yaani kupiga kura) na kuchaguliwa (yaani kupigiwa kura) kwenye nafasi yoyote katika chama

d) Haki ya kujitetea dhidi ya jambo lolote linalomkabiri katika uhusiano wake na wanachama wengine au juu ya mwenendo wake kwa ujumla.

e) Haki ya kutoa hoja yoyote inayohusu mwenendo wa wanachama ndani ya mikutano ya chama

f) Haki ya kujitoa kwa hiari kwenye chama

### 3.1.5. Ukomo wa Uanachama

Hamu ya wanachama ni kuhimizana ili asipotee mwanachama hata mmoja kwa kupoteza sifa za uanachama. Hata hivyo mambo yafuatayo yakitokea yatasababisha ukomo wa uanachama:

a) Mwanachama kujiuzulu au kuomba kuacha uanachama yeye mwenyewe kwa sababu zozote zile.

b) Kuasi imani Katoliki

c) Kukosa sifa za uanachama, kuvunja masharti ya chama na kuacha kutimiza wajibu wa mwanachama kadiri ya mwongozo au maamuzi yoyote ya pamoja.

## 3.2. MALEZI

### 3.2.1. Malezi ya Awali

Mkristo mkatoliki anapoguswa na maisha ya chama na kuonyesha hamu na nia ya kujiunga, atakaribishwa kuanza kushiriki maisha ndani ya chama na kupewa malezi ya awali kwa kufuata mada zifuatazo:

a) Uelewa wa Chama na Utume wa Damu kwa ujumla.

b) Alama za Tasaufi ya Damu: Agano, Msalaba, Kikombe, Mwanakondoo na Upatanisho

c) Nguzo Tatu za Shirika.

d) Historia ya Shirika.

e) Mt. Gaspari del Bufalo, Mt. Maria de Mattias na Mtumishi wa Mungu Giovanni Merlini.

f) Mafundisho ya Kanisa kuhusu Damu Azizi.

g) Changamoto za Utume wa Damu Azizi leo.

### 3.2.2. Kupokelewa Rasmi na Daima

a) Mwanachama mpya atapokelewa rasmi na kwa daima katika chama baada ya kumaliza malezi ya awali.

b) Muda wa kupokelewa rasmi katika chama itakuwa miaka miwili baada ya kuanza malezi ya awali.

c) Mwanachama mpya atapokelewa rasmi katika chama kwa ibada maalum itakayofanyika ndani ya Misa Takatifu (Angalia Ibada katika Viambatisho).

d) Wanachama wapya watapokelewa katika kanda zao wakati wa Sherehe ya Damu Azizi mwezi wa Julai.

#### 3.2.3. Malezi Endelevu

a) Baada ya mwanachama kupokelewa rasmi na kwa daima katika chama, atapata fursa ya malezi endelevu ndani ya chama kwa njia ya Mafungo, Semina na Maisha ya Sala.

b) Wanachama watarudia Ahadi za Uanachama kila mwaka wakati wa Sherehe ya Damu Azizi mwezi Julai.

## 4. SEHEMU YA NNE

### 4.1. MUUNDO WA CHAMA

a) Chama kitagawanyika katika ngazi tatu kama ifuatavyo kutegemeana na mazingira ya mahali:

   i) Ngazi ya Tawi
   ii) Ngazi ya Kanda
   iii) Ngazi ya Provinsi

b) Kwa kuwa wanachama wapya watapatikana kutokana na mahusiano yao na Shirika au na chama, muundo wa chama ngazi za Tawi utategemea aina ya mahusiano yaliyopo. Kwa mfano Waseminari wa zamani wa Shirika (*Ex Seminarians*), wanaparokia au wafanyakazi wa taasisi fulani.

### 4.2. UONGOZI

#### 4.2.1. Mfumo wa Uongozi

a) Chama kitakuwa na viongozi wa kuchaguliwa katika ngazi zote tatu kama ifuatavyo:

   i) Mwenyekiti
   ii) Makamu Mwenyekiti
   iii) Katibu
   iv) Katibu Msaidizi
   v) Mweka Hazina

b) Kutakuwa na kiongozi wa Ibada na liturjia katika ngazi ya Tawi atakayeteuliwa na Mwenyekiti wa Tawi kulingana na vipaji alivyonavyo vya kiibada.

c) Kiongozi wa Ibada au liturjia ngazi ya Kanda atachaguliwa kwa kupigiwa kura katika kikao cha viongozi wa ibada wa Matawi yote katika Kanda husika.

d) Kiongozi wa ibada katika ngazi ya Provinsi atachaguliwa kwa kupigiwa kura katika kikao cha viongozi wa ibada wa Kanda zote za Provinsi.

e) Kutakuwa na mlezi wa chama ambaye ni mmisionari wa Damu Azizi atakayeteuliwa na Mkuu wa Shirika, Provinsi ya Tanzania; atashika wadhifa huo kwa muda utakaoelekezwa na Mkuu wa Shirika.

f) Muda wa uongozi ni miaka miwili (2)

g) Uchaguzi mdogo unaweza kufanyika endapo kiongozi / viongozi watashindwa kutimiza wajibu wao kadiri ya mwongozo au kujihuzulu wenyewe.

h) Viongozi waliomaliza muda wao wanaweza kuchaguliwa tena lakini wasiwe wamekalia nafasi hiyo hiyo kwa zaidi ya vipindi vitatu mfululizo.

i) Huduma ya uongozi katika chama haiishii tu kwa hawa viongozi watano na mlezi, bali kila mwanachama lazima ajione kuwa ni kiongozi na anawajibika kubuni namna ya kukifanya chama kiendelee kukua (C49).

### 4.2.2. Wajibu na Kazi za Viongozi

**a) Mlezi wa Chama**

i) Kutoa ushauri na maelekezo mbalimbali kadiri ya wadhifa wake.
ii) Kuhakikisha chama kinafikia malengo yaliyokusudiwa.
iii) Kuwa kiungo kati ya chama na Shirika.
iv) Kuhakikisha chama kinashirikiana na vikundi vingine vya walei na wasio walei katika kazi za kitume katika Kanisa.
v) Kuhudhuria vikao vya chama na kutimiza wajibu mbalimbali kadri atakavyoagizwa na wakubwa wake.
vi) Kuhudhuria sala na ibada mbalimbali za chama kadiri muda utavyomruhusu.
vii) Hatakuwa na haki ya kupiga kura katika uchaguzi wowote lakini ataweza kutoa uamuzi wa mwisho pale panapotokea utata hasa katika uchaguzi.

**b) Mwenyekiti / Makamu Mwenyekiti**

i) Atakuwa msemaji mkuu wa chama katika ngazi husika ya uongozi
ii) Ni kiongozi na msimamizi wa shughuli zote za chama akishirikiana na mlezi.
iii) Atahakikisha chama kinaimarika na kusimamia mwongozo kikamilifu
iv) Ni mwenyekiti wa vikao vyote vya chama katika ngazi husika

**c) Katibu / Katibu Msaidizi**

i) Ni katibu mkuu mtendaji wa chama katika ngazi husika
ii) Ni mwandishi na mwekaji wa kumbukumbu za vikao vyote vya chama katika ngazi husika
iii) Ni mtayarishaji wa taratibu zote za chama kwa kushirikiana na mwenyekiti
iv) Mfuatiliaji wa maazimio na mipango ya chama katika ngazi husika
v) Mwandishi mkuu wa barua au taarifa nyingine zinazohusu chama katika ngazi husika

**d) Mweka Hazina**

i) Mtunza fedha na taarifa zote za fedha za chama katika ngazi husika.
ii) Ni mtoaji wa taarifa zote zihusuzo mapato na matumizi ya chama.
iii) Ni mtengenezaji / mwandaaji wa bajeti ya chama katika ngazi husika.
iv) Mweka Hazina wa ngazi ya Tawi atafuatilia na kuwakumbusha wanachama wajibu wao wa kutoa michango iliyopangwa na chama.
v) Kutoa taarifa ya mapato na matumizi ya chama katika ngazi husika wakati wowote inapohitajika.
vi) Kutoa taarifa za dharura zinazohusu mfuko wa chama katika ngazi husika.

vii) Mweka Hazina wa ngazi ya Kanda atafuatilia michango kutoka kwenye Matawi yaliyo katika Kanda yake kadiri itakavyokuwa imeamriwa na chama.

viii) Mweka hazina wa ngazi ya Provinsi atafuatilia michango kutoka kwenye Kanda zote kadiri itakavyokuwa imepangwa na chama.

### 4.2.3. Kusitishwa kwa Uongozi

a) Uongozi / Kiongozi unaweza / anaweza kusitishwa wakati wowote kabla ya muda wa uongozi kuisha iwapo:

i) Uanachama wake umefikia ukomo (angalia kipengele 3.1.5 cha mwongozo huu)

ii) Kumekuwa na kutokuwajibika ipasavyo kuleta maendeleo ya chama kwa mujibu wa taratibu za chama.

iii) Wanachama watakosa imani nao / naye kwa idadi ya theluthi mbili ya wanachama wote katika ngazi husika.

iv) Ataamua kujiuzulu kwa ridhaa yake mwenyewe kwa maslahi ya chama; na zaidi ya nusu ya wanachama katika ngazi husika wamekubaliana na ombi lake la kujihuzulu.

## 4.3. VIKAO

a) Kila ngazi ya chama itakuwa na vikao kama ifuatavyo:

i) Kikao cha Tawi: Kitaitishwa na mwenyekiti wa Tawi na kitafanyika mara moja kila mwezi; kitahudhuriwa na wanachama wote wa Tawi husika.

ii) Kikao cha Kanda: Kitaitishwa na Mwenyekiti ngazi ya Kanda na kitafanyika mara mbili kwa mwaka na kitahudhuriwa na wanachama wote wa Kanda husika.

iii) Mkutano Mkuu: Utaiitishwa na Mwenyekiti ngazi ya Provinsi na utafanyika mara moja kwa mwaka; utahudhuriwa na viongozi sita wa kila Tawi, watano wa Kanda na viongozi ngazi ya Provinsi.

# 5. SEHEMU YA TANO

## 5.1. IBADA NA SALA

Licha ya ibada na sala zinazoelekezwa kwa maisha ya mkristo kwa ujumla, mwanachama atajibidisha kufanya yafuatayo:

a) Kuabudu Ekaristi Takatifu walau mara moja kwa mwezi.

b) Kusali kila siku sala za chama kadiri ya Mto wa Rehema.

c) Kusali Novena ya Damu Azizi kabla ya Sherehe ya Damu Azizi.

d) Kuhudhuria Misa kwa heshima ya Damu Azizi ya Yesu kila Ijumaa.

e) Kuhudhuria maadhimisho ya Sherehe ya Damu Azizi ya Yesu tarehe 1 Julai.

f) Kufanya tafakari ya Damu Azizi katika Mwezi wa Damu Azizi (Julai).

g) Kuhudhuria maadhimisho ya Sherehe ya Mt. Gaspari Del Bufalo tarehe 21 Oktoba.

h) Kufanya Hija mara moja kwa mwaka katika makanisa au vituo vya hija.

i) Kupokea sakramenti ya upatanisho mara kwa mara.

### 5.2. UTUME

Utume wa wanachama utakuwa kama ifuatavyo:

a) Wanachama wanashiriki utume wa Kanisa na wa Shirika wa kutangaza fumbo la Kristo la kumwaga damu yake akawakomboa na kuwapatanisha wanadamu wote waweze kushiriki Ufalme wa Mungu (C21).

b) Kutoa ushuhuda wa Neno la Mungu kimaisha kwa kuchota nguvu kutoka Tasaufi ya Damu Azizi, Maandiko Matakatifu, Ibada, Sala na Mafundisho ya kanisa (C23, 24).

c) Kwa kufuata karama ya Mt. Gaspari Del Bufalo, wanachama wanajibidisha kutambua hali na mahitaji ya watu (Kilio cha damu) na kutafuta namna ya kuwasaidia (Kujibu kilio cha damu) (C22).

## 6. SEHEMU YA SITA

### 6.1. MICHANGO

#### 6.1.1. Mchango wa Kiingilio

a) Mwanachama mtarajiwa anapoanza malezi ya awali katika chama atatakiwa kutoa mchango wa kiingilio kiasi kitakachokuwa kimepangwa na chama.

#### 6.1.2. Ada ya Mwaka

a) Mwanachama na mwanachama mtarajiwa atatakiwa kulipa ada ya mwaka kiasi kitakachopangwa na chama ndani ya mwezi Januari kila mwaka.

b) Mweka Hazina wa ngazi ya Tawi atatoa taarifa ya michango yote iliyokusanywa siku ya kikao cha kwanza katika mwaka unaoanza.

#### 6.1.3. Michango Mingine

a) Chama kitakuwa na michango mingine kadiri ya mahitaji ya utume na matendo ya huruma kwa wahitaji kadiri itakavyopitishwa na chama.

## 7. VIAMBATISHO

### 7.1. IBADA YA KUPOKELEWA WANACHAMA WAPYA

*(Ibada hii ikifanyika katika Misa Takatifu, hufanyika baada ya masomo na homilia)*

**UTAMBULISHO *(Mlezi)*:**

1. Wale wanaotaka (Yule anayetaka) kujiunga na Utume wa Walei wa Damu Azizi wajongee (ajongee) mbele *(Anawaita majina na kila mmoja anapoitwa jina anaitika kwa kusema, "Nipo")*

**OMBI *(Watakaji)*:**

2. Baba Mkuu (Mwakilishi wa Mkuu) wa Shirika la Wamisionari wa Damu Azizi ya Yesu, mimi __________________, baada ya tafakari ya muda mrefu juu ya wito wangu, Malezi katika utume wa Walei wa Damu Azizi, semina, mafungo na ibada mbalimbali za Damu Azizi na mahusiano ya karibu na Wamisionari wa Damu Azizi, naomba kujiunga kwa daima katika Utume wa Walei wa Damu Azizi na ninaahidi kuishi kikamilifu karama ya kimisionari, tasaufi ya Damu Azizi na Utume wa kueneza upendo wa Damu katika maisha yangu, nikifuata katiba ya utume na maelekezo ya Shirika la Damu Azizi ya Yesu.

**KUPOKEA OMBI *(Mkuu wa Shirika / Mwakilishi)*:**

3. Mimi, _________________, Mkuu wa Shirika (Mwakilishi wa Mkuu wa Shirika) la Wamisionari wa Damu Azizi, Provinsi ya Tanzania, nawapokea rasmi kila mmoja wenu (nakupokea rasmi) katika Utume wa Walei wa Damu Azizi ya Yesu.

   Kwa maneno ya Mt. Gaspar del Bufalo Mwasisi wetu, "Tunaomba Damu ya Yesu Kristo ituimarishe kikwelikweli." Tafakari yenu (yako) ya Mada za Mafunzo ya Maandalizi, pamoja na ushirikiano wenu (wako) na Wanachama wengine wa Utume wa Damu, Marafiki wa Shirika, Wamisionari wa Damu Azizi na Maisha ya Utume kwa pamoja viwapatie (vikupatie) mwanga na uelewa mpevu kuhusu wito wenu (wako) wa kueneza upendo wa Damu ili muweze (uweze) kuuitikia kwa uaminifu mahali popote.

   Nawahakikishieni kuwa mtapata msaada wa maombezi wakati wote kutoka kwa Wanachama wengine wa Utume wa Damu, na Marafiki na Wamisionari wa Damu Azizi.

   Karibuni sana!
   *(Kupokelewa huashiriwa kwa kupiga makofi).*

**KUJIWEKA WAKFU KWA DAMU YA YESU *(Watakaji)*:**

***(Wakiwa wamepiga (akiwa amepiga) magoti wanasali kwa pamoja)***

4. Tunakushukuru, Bwana Yesu Kristo kwa kujifanya mtu na kuleta pendo la Baba wa mbinguni katika ulimwengu wetu. Tunakushukuru, Mwana wa Mungu, kwa kutwaa mwili na damu yetu, na kuwa ndugu na rafiki yetu. Tunakushukuru, mchungaji mwema, kwa kuutoa uhai wako kwa ajili ya kundi lako, ili kuwaosha na kuwatakasa wale wanaopokea neno lako na kuwa washiriki wa sadaka yako ya upatanisho.

Pamoja na malaika na watakatifu wote tunakusifu na kukutukuza, Ee Bwana, kwa kuondoa kosa la wanadamu kwa Damu yako Azizi. Tunakuheshimu na kukutukuza kwa kutupatia tumaini jipya kwa kutoa maisha yako: kifo kwetu sasa ni mlango wa ufufuko, na katika huruma uliyotuonesha, tukiungana nawe, sisi nasi twaweza kuwa chanzo cha huruma na upatanisho.

Tunakusifu na kukutukuza, Mwokozi wetu, kwa kuwa kwa njia ya Ubatizo na Kipaimara unatufanya viungo vya mwili wako mtakatifu, yaani Kanisa; kwa njia ya Ekaristi Takatifu unatuunganisha katika muungano wa upendo na amani, na kwa njia ya Sakramenti ya Upatanisho unaponya majeraha yetu sisi tunaosafiri duniani, na kuturudishia upya maisha ya neema.

Tunakushukuru na kukutukuza, Ee Yesu, kwa Neno lako na Sakramenti zote, ambazo hutufanya viungo hai vya Kanisa.

Tunakushukuru kwa ajili ya wale wanaoongoza kundi lako ulilolilunganisha kwa Damu yako. Shukrani zitolewe kwako, Ee Bwana, kwa ajili ya wote waliotusaidia kupata imani, na kwa wale waliotuongoza katika njia ya pendo lako.

Tunakushukuru kwa namna ya pekee leo, kwa kuwa katika Damu yako tumegundua maana ya fumbo la maisha, mateso na kifo. Jinsi ulivyoshiriki maisha yetu kwa upendo, ukateswa na ukafa msalabani, hivyo nasi tunamtolea Mungu Baba pamoja nawe maisha yetu, mateso na hata kifo chetu, ili tuwapende ndugu zetu kama wewe ulivyotupenda sisi.

Kwa hiyo leo tunajitolea kwako, tuwekwe wakfu tena kwa njia ya Damu yako Azizi. Tunarudia upya ahadi za Ubatizo na tuna hamu ya kuimarika zaidi na kuwa zaidi viungo hai vya mwili wako, Kanisa. Tunataka maisha yetu yasaidie kukamilisha kile kinachopungua katika ukombozi na wokovu wa ulimwengu. Tunapenda muda wetu uwe muda wako, furaha yetu iwe furaha yako, na mateso yetu yashiriki katika pendo lako la ukombozi. Pamoja nawe tuwe tayari kutoa damu yetu, na hata uhai wetu kwa ukombozi wa ulimwengu.

Ee Bwana, tujalie kuwa pamoja nawe chemchemi ya huruma, ili tushinde woga na roho mbaya; tuwape nguvu mpya waliopo hatarini au waliojeruhiwa; tuwafariji wenye huzuni; tuonesha njia ya ukweli kwa wanaoitafuta; tuwahimize wakosefu wakurudie; tuwaimarishe waliojitolea kwako; tuwahudumie wanaokufa na tuwaombee marehemu katika kujitakasa kwao.

Ee Bwana Yesu Kristo, kwa ajili ya Damu yako Azizi, utujalie kuishi kiaminifu katika tendo hili la kujiweka wakfu kwako. Utufanye waabudu wa fumbo la upendo wako. Utujalie nguvu ya kutoa ushuhuda wa wito wetu, ili watu wengi zaidi washiriki katika kuabudu Damu yako Azizi na kuungana nasi katika maisha ya kumtukuza Mungu na kujitolea kwa watu. Amina!

**SALA** ***(Mkuu au Mwakilishi wa Shirika):***

5. Bwana Yesu, uliyewachagua mitume na kuwaagiza waende duniani kote kuihuribi Injili kwa kila kiumbe (Mk. 16:15) na ukawaagiza wawe mashahidi wako (Mdo. 1:8), tunawaombea hawa wanachama wapya wa utume wa Walei wa Damu Azizi, uwaongoze katika wito wao, waendelee kutambua wajibu wao na wasikate tamaa katika kukabiliana na changamoto za kiutume. Unayeishi na kutawala daima na milele, Amina.

**KUPEWA ALAMA:**

*(Mkuu wa Shirika au Mwakilishi anawapa wanachama wapya kila mmoja Tasbihi ya Damu Azizi, kitabu cha Damu ya Kristo Mto wa Rehema na beji ya chama)*

6. Pokea Tasbihi hii ya Damu Azizi na kitabu cha Damu ya Kristo Mto wa Rehema viwe alama ya uwanachama wako na vikusaidie katika sala na ibada kwa Damu Azizi.

**KUSAINI AGANO:**

*(Mwanachama mpya na Mkuu wa Shirika / Mwakilishi wanasaini hapo chini)*

**Mwanachama:**

______________________________ *(Jina)* ________________ *(Saini)*

**Mkuu / Mwakilishi wa Mkuu wa Shirika:**

__________________ *(Jina)* ________________ *(Saini)*